

*Sekta ya Uvuvu kuipaisha Singida kimapato *

Na Elisante John, SINGIDA

MANISPAA ya Singida imeanza kuimarisha vyanzo vyake vya mapato vya ndani, tkiwamo sekta ya uvuvu katika mabwawa makabwa mawili, maarufu Ziwa Singidani na Kindai, yaliyoko pembezoni mwa mji wa Singida.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema jana kuwa ili sekta hiyo ichangie kikamilifu pato la ndani, shughuli za uvuvu ndani ya Ziwa Kindai na Singidani kwa muda wa miezi mitano zitasitishwa ili kupisha samaki kuzaliana na wauvu kukata leseni mpya.

Alisema ili kudhibihi shughuli

za uvuvu, wameanza msako na tayari wamekamata wavuvi kadhaa na nyavu, huku akiahidi jambo hilo ililoanza Januari 31, hadi Mei 31, mwaka huu, litakuwa endelevu.

Katika msako huo unaojumuisha maofisa wa idara za uvuvu, biashara na askari mgambo, Nipashe ilishuhuda nyavu nne kubwa na mitumbwi miwili ikiwa imekamatwa baada ya kutelekezwa na wavuvi wanaokaldi zuio hilo.

"Maziwa haya mawili yana mehangi mkubwa kwa uchumi wa mji wetu. Hatuwezi kuyaacha hivi hivi kipindi hildi. Sasa samaki wakubwa wanaoishi kwenye kina kirefu wanazimika kuja juu

kutafuta matingatinga katika kina kifupi ili kutaga mayai," alisema.

Katika kuhakikisha manispaa inafanikisha zuio hilo, alisema wanatarajia kupokea boti moja kutoka bonde la kati la maji, itakayotumika mchana na usiku hasa katika Ziwa Kindai ili kudhibiti wavuvi wasiotaka kuttii taratibu na sheria.

Aidha, Lupembe alifanua kuwa, tayari kikosi kazi maalum kimeundwa kwa ajili ya kufanya msako wakati wowote mchana na usiku, ili wale wote watakoshindwa kutfi zuio hilo, wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Alibainisha kipindi hiki am-

bacho ziwa limefungwa, wavuvi watumie nafasi hili kwenda kujata leseni ya uvuvu, kwa ajili ya kurahisisha shughuli za uvuvu na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za nchi.

Ofisa Mifugo na Uvuvu Manispaa ya Singida, Dk. Adrianus Kalekezi, alisema Ziwa Singida na Kindai yana wavuvi 150 wanaoweza kuongeza mapato ya ndani, kutokana na malipo ya ushuru na kodi, pla kwa leseni mpya watakazokata.

Dk. Kalekezi alisema maziwa hayo yenye samaki aina ya perege na furu, yana idadi hiyo ya wavuvi ambao kati ya Juni hadi Desemba, mwaka jana, wali-

ingizia manispaa mapato ya Sh. milioni 280 kutokana na tani 35 za samaki.

Mmoja wa wavuvi, Salum Kikokomeko, anayevua samaki katika maziwa hayo kwa muda nirefu sasa, alisema kuryafunga maziwa hayo ni kuwasumbua wavuvi kwa kuwa wengi wao ni wa kipato cha chini kutokana na zana dunii wanazotumia wakati samaki walijoko ni wengi.

Kutokana na hali hiyo, Kikokomeko alitumia fursa hiyo kuiomba Manispaa ya Singida, kujutana na wavuvi mara kwa mara, ili kubadilishana mawazo yenye nia ya kuleta tija baina ya pande zote.